

Hitimisho Kuhusu **الْوَقْفُ وَالْإِبْتِدَاءُ** Al-Waqfu wal-Ibtidaai (Kisimamo na Kianzio):

Wanavyuoni wamekubaliana yafuatayo kuhusiana na somo hili la **الْوَقْفُ وَالْإِبْتِدَاءُ** Al-Waqfu wal-Ibtidaai (Kisimamo na Kianzio):

1. Kusimama katika mwisho wa Aayah ni Sunnah iliyothibiti kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم):
2. Hakuna katika Qur-aan kisimamo cha kuwajibika au cha haraam isipokuwa kile kinachoharibu maana.

Kwa mwanafunzi wa kawaida anayetaka kujisalimisha na kosa la kusimama katika neno litakaloharibu au kupotosha maana iliyokusudiwa, anaweza kusimama popote apendapo katika alama zozote za Qur-aan isipokuwa tu asisimame katika alama ya لا. Na pia asisimame katikati ambako hakuna alama yoyote kwa sababu aghlabu kusimama kwenye neno lisokuwa na alama huenda ikawa ni 'Kisimamo Kinachochukiza' kutokana na upungufu katika uhusiano baina ya maneno mawili kimaana na kilugha na hivyo hata kuanzia kwake neno la pili likawa ni kosa kubwa katika kuanzia kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى). Mifano:

1. Kusimama katika neno: **وَتَسْبِيحُهُ** katika kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى):

لِتُؤْمِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَتُعَزِّرُوهُ وَتُوَقِّرُوهُ وَتُسَبِّحُوهُ بُكْرَةً وَأَصِيلاً

((Ili [nyinyi] mumwamini Allaah na Rasuli Wake, na mumsaidie na mumheshimu (Mtume Muhammad صلى الله عليه وسلم) na mumsabbih (Allaah سبحانه وتعالى) asubuhi na jioni.))¹

Kwa sababu atakaposimama kwenye neno hilo, huenda ikafahamika kwamba kitendo hicho cha "kusabbih" (kumtakasa Allaah)

¹ Al-Fat-h (48: 9)

kinaungana na viwili vilotajwa nyuma yake vya ‘kumsaidia na kumheshimu Mtume صلى الله عليه وسلم” na hali hapo maana ya “kusabbih” inamrudia Allaah (سبحانه وتعالى) Ambaye Aameanzwa kutajwa katika Aayah.

2. Kusimama katika neno: **لَا تُشْرِكْ** katika kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى):

وَإِذْ قَالَ لُقْمَانُ لِابْنِهِ وَهُوَ يَعِظُهُ يَا بُنَيَّ لَا تُشْرِكْ بِاللَّهِ إِنَّ الشِّرْكَ لَظُلْمٌ عَظِيمٌ ﴿٣١﴾

((Na [kumbusha pale] Luqmaan alipomwambia mwanawe huku akimuwaidhi: “Ee mwanangu! Usimshirikishe Allaah, hakika shirki ni dhulma kubwa mno!”))²

Kwa sababu ikisimamiwa neno hilo na kuanziwa linalofuatia: **بِاللَّهِ**

Italeta maana kwamba msomaji anaanza kuapia kwa jina la Allaah (سبحانه وتعالى) na hali lilokusudiwa ni: **لَا تُشْرِكْ بِاللَّهِ** (Usimshirikishe Allaah)

Hiyo ni mifano miwili miongoni mwa mingi, na pindi msomaji atakaposimamia neno ambalo halikuwekewa alama basi ni vyema arudie maneno ya nyuma ili aunganishe na yanayofuatia hadi afikie kwenye alama inayoruhusu kusimama.

² Luqmaan (31: 13)